**BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA**

**MTIHANI WA UTAMILIFU WA SHULE ZA KIISLAMU**

**KIDATO CHA PILI**

**HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI**

**060 MWONGOZO WA USAHIHISHAJI JULAI/AGOSTI, 2026**

**SEHEMU A (ALAMA 15)**

(Jibu maswali yote katika sehemu hii

1.

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| C | C | A | C | D | D | B | C | A | B |

**Alama 01 @ swali = Alama 10**

2.

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|
| C | E | F | A | B |

**Alama 01 @ swaliu = Alama 05**

**SEHEMU B (ALAMA 70)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii

3. Sababu zilizopelekea kuhama na mtawanyiko wa jamii za Kiafrika.

(i) Sababu za kibiashara

(ii) Kutafuta ardhi yenye rutuba

(iii) Kupasuka kwa koo zao

(iv) Kutokea majanga ya asili kama vile ukame, mafuriko na njaa kali

(v) Sababu za kihusiano kama vile kuoa na kuolewa

**Alama 02 @ hoja = Alama 10**

Shulelibrary.com

4. Jumuiya, taasisi na vyama vilivyopambana kutafuta uhuru nchini Tanganyika:

(i) Vyama vya ushirika na wakulima mfano: Bukoba Buhaya Union ( 1924)

(ii) Vyama vya wafanyakazi mfano: Tanganyika Territory Civil Servants Association (TTCSA)

(iii) Vyama vya wafanyabiashara mfano: African Commercial Association (1934)

(iv) Vikundi vya vyama vya kidini mfano: Aljaamiatul Islamiyya fi Tanganyika (1933)

(v) Vilabu vya mipira ya miguu mfano: The African Sports Club

(vi) Vyombo vya habari mfano: Gazeti la Sauti ya TANU

(vii) Vyama vya siasa mfano: African Association (AA) 1929

**Hoja 05 alama 02 @ Hoja = Alama 10**

5. Matokeo ya ugunduzi wa chuma

(i) Uliboresha ulinzi na usalama kutokana na utengenezaji wa silaha mti mikuki

(ii) Kukua kwa sekta ya kilimo kutokana na utengenezaji wa zama za kilimo kama vile majembe na mapanga

(iii) Ukuaji wa biashara kwa kuwa bidhaa za kubadilishana ziliongezeka

(iv) Ulisaidia ubunifu wa zama mbalimbali kama vile visu n.k.

(v) Ukuaji wa miji iliyopata umaarufu katika kufua vyuma

(vi) Ulisaidia kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla.

**Hoja 05 alama @ hoja = Alama 10**

6. Umuhimu wa Mapinduzi ya Zanzibar:

(i) Kujenga umoja. Migawanyo na chuki zilizojengwa na ukoloni zilisambaratishwa

(ii) Yalichochea muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar. Muungano huu uliwaleta pamoja watu kutoka asili na kenda mbalimbali na kuleta utambulisho wa kitaifa.

(iii) Kuleta na kujenga mshikamano. Mapinduzi haya yalileta mshikamano wa kitaifa.

(iv) Serikali ya Zanzibar ilipitisha kanuni za ujamaa na udugu ambazo zilileta usawa, umiliki wa pamoja wa rasilimali na mshikamano.

Shulelibrary.com

(v) Mapinduzi haya yalichochea hisia ya fahari ya kitaifa, uzalendo na kujitolea ambayo yameendelea kujenga mfumo wa maadili wa taifa hadi sasa.

**Alama 02 @ Hoja = Alama 10**

7. Umuhimu wa kutunza maeneo yenye urithi wa asili na kihistoria:

(i) Kuongeza shughuli za utalii na fedha mfano: Utalii katika mbuga za wanyama

(ii) Urithi huu unasaidia kutunza utamaduni. Kuhifadhi vitu vya asili na kihistoria ni ishara ya kuthamini utamaduni wetu

(iii) Kujenga mshiakamano, ushirikiano na umoja mfano: Kupitia shughuli za kiutamaduni

(iv) Kudumisha mila na desturi kupitia hifadhi mbalimbali za kihistoria na kiasili

(v) Kutoa elimu na maarifa. Kupitia masimulizi ya asili mafunzo mbalimbali hupatikana.

**Alama 02 @ Hoja = Alama 10**

8. Matokeo ya kuupinga uvamizi wa kikoloni miongoni mwa jamii za Kitanzania:

(i) Kusimama kwa shughuli za uzalishaji mali, hii ni kutokana na vita vya mra kwa mara.

(ii) Wenyeji kutumikishwa kwa nguvu katika mashamba ya walowezi hasa hasa nguvukazi ya vijana.

(iii) Vifo vingi kutokana na wanyamapori, hii ni kwa sababu wapiganaji wa Kiafrika walitumia muda mwingi kujificha msituni.

(iv) Hofu kubwa kutanda miongoni mwa Watanzania

(v) Watanzania kupata mateso na vifo vingi, hii ni kutokana na sababu mbalimbali kama vile njaa, kunyongwa, kukamatwa na kuwa mateka n.k.

(vi) Kupatikana mwamko mpya wa harakati za uhuru, upingaji wa uvamizi huu uliacha alama iliyopelekea kuleta morali wa kupigania uhuru hapo baadaye.

(vii) Kuacha kumbukumbu muhimu katika historia ya Tanzania.

**Hoja 05 alama 02 @ Hoja = Alama 10**

shulelibrary.com

9. Umuhimu wa ngoma za asili na michezo ya jadi katika jamii za Kitanzania:

(i) Kuburudisha

(ii) Kuwaunganisha wanajamii

(iii) Kujenga ujasiri

(iv) Kujenga uzalendo

(v) Kudumisha amani

(vi) Kuelimisha

**Hoja 05, alama 02 @ Hoja = Alama 10**

**SEHEMU C (Alama 15)**

Jibu swali la kumi (10)

10. **Utangulizi**

Mwanafunzi anatakiwa aeleze maana ya maadili.

Maadili ni miongozo inayotawala tabia na matendo ya mtu mmojammoja au jamii kwa ujumla.

**Kiini**

Maadili yaliyodumishwa wakati wa ukoloni.

(i) Umoja na ushirikiano mfano: Kilimo cha jumuiya

(ii) Heshima kwa wazee mfano: Kuwapokea mizigo na kuwasalimia

(iii) Mifumo ya haki ya jadi mfano: Kuwepo mabaraza ya usuluhishi

(iv) Ukarimu mfano: Kuwakarimu wageni kwa kuwapa chakula

(v) Utii kwa mamlaka, heshima kwa uongozi wa ndani na miundo ya kimila

(vi) Utamaduni wa masimulizi. Mfano: Matumizi ya hadithi, methali na hekaya katika kutoa elimu.

**Hitimisho**

Kueleza dhana yoyote inayohusiana na dhana ya maadili ya Waafrika.

**Utangulizi: Alama 03**

**Kiini hoja: Alama 05 @ hoja alama 02 = Alama 10**

**Hitimisho: Alama 02**

Shulelibrary.com